

Jarida la _____ Toleo Na. 6
SAMIA TENA
05/09/2025 2025-2030



NJOMBE NA RUNGWWE

ZASIMAMA KAMPENI ZA SAMIA





RAIS SAMIA KUANZISHA VIWANDA 50 VYA KUHIFADHI ZAO LA PARACHICHI NA MBOGAMBOGA NCHINI

Mgombea urais kupitia Chama Cha Mapinduzi(CCM) na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dkt Samia Suluhu Hassan amesema iwapo atapewa ridhaa ya kuongoza tena kipindi kingine atajenga viwanda 50 vya kuhifadhi parachichi na mbogamboga ili kulinda zao hilo lisiharibike wakati wa utafutaji wa soko lake nje ya nchi.

Rais Samia ameyasema hayo leo Rungwe wakati akihutubia maelfu ya wananchi waliofika kusikiliza kampeini za kunadi ilani ya CCM.

Rais Samia amesema kati ya viwanda hivyo 50, viwili vitajengwa Rungwe.

Rais Samia amesema viwanda hivi vitahifadhi mazao haya kwa miezi mitatu wakati wakulima wakitafuta soko ambalo kimsingi limeshuka kutokana na ushindani wa uzalishaji wa zao hilo katika nchi nyingine kama za Afrika Kusini na Kenya ambao kwa Afrika ndo vinara na Tanzania ikiwa ni ya tatu.

Sambamba na hilo, Rais Samia amesema ili kulipa zao hilo thamani, serikali itaanzisha kongani za viwanda ambazo zitasaidia kujengea viwanda vijana ambavyo vitatumika kuongeza thamani ya zao la parachichi kama kuzalisha mafuta na mambo mengine ili kulipa thamani zaidi zao hilo nchini.

Katika kuhakikisha zao la parachichi linachangia uchumi nchini, Rais Samia amesema watanunua miche milioni moja na kuwapa wakulima bure ili kuongeza uzalishaji wake nchini.

Rais Samia amesema ataajiri pia maafisa ugani wa zao hilo ili kusaidia wakulima kupima udongo na kutoa ushauri mzuri wa namna na kuzalisha zao hilo kwa wingi.

Rais Samia pia amesema atahakikisha wakulima wa parachichi wanapata ruzuku ya mbolea bure na dawa ya kukuzia zao hilo. Ameongeza kuwa tayari serikali ilishanunua dawa ya zaidi ya bilioni mbili kwa ajili hiyo.



SERIKALI KUMILIKISHA MASHAMBA YA CHAI YA 'MOHAMMED ENTERPRISES TANZANIA LTD' KWA VYAMA VYA USHIRIKA

Mgombea urais kupitia Chama Cha Mapinduzi (CCM) na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dkt Samia Hassan Suluhu amesema iwapo atapata ridhaa ya kuongoza kipindi kingine atamilikisha mashamba ya chai ya Mohammed Enterprises Tanzania Limited (MeTL) na Kiwanda cha Wakulima cha Wakulima Tea Company Limited (WATCO) kwa vyama vya ushirika ili kuendesha rasilimali hizo kwa ufanisi na faida kwa wananchi.

Rais Samia ameyasema leo wakati akihutubia wananchi waliodhuria kampeini zake za kuomba kuchaguliwa tena wilayani Rungwe.

Rais amesema sababu kufanya hivyo ni kwa wamiliki wa mashamba hayo kutoyaendeleza kama walivyokuwa wamekubaliana na serikali.

Rais Samia amesema mashamba hayo serikali iliyatoa kwa sekta hizo binafsi na kuwawekea mazingira mazuri sana lakini mategemeo hayakuwa kama ilivyokuwa imepangwa.

Kutokana na hilo, Rais Samia amesema serikali imeunda timu ya tathmini ya mashamba na viwanda ili ni kuona ni kwa namna gani yatamilikishwa kwa vyama vya ushirika.

Sambamba na hilo, Rais Samia amesema wenye mashamba na viwanda hivyo wameelekezwa kulipa madeni ya wakulima kabla ya serikali kutachukua.

Kwa muda mrefu kumekuwa na kelele nyingi kutoka kwa serikali na wananchi kuwa mashamba mengi ya MeTL yametelekezwa na kuwa mapori badala ya kuendelezwa kwa manufaa ya nchi na wananchi.

Taarifa kutoka vyanzo mbalimbali vya wilaya vinasema shamba la MeTL wamekuwa wanazalisha kilo 900 tu kwa hekta moja katika shamba lenye ukubwa wa hekta 1150, ambalo hekta zao 500 haziendelezwi.





RAIS SAMIA KUUNGANISHA UMEME KATIKA VITONGOJI 712 VYA WILAYA YA MBARALI

Mgombea urais kupitia Chama Cha Mapinduzi (CCM) na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dkt Samia Suluhu Hassan amesema iwapo atapewa ridhaa ya kuongoza tena atahakikisha vitongoji vyote 712 vya wilaya ya Mbarali vinaunganishwa umeme.

Rais Samia ameyasema hayo leo wilayani Mbarali wakati akihutubia maelfu ya wafuasi wa CCM waliofika kusikiliza sera za chama chake kuelekea uchaguzi mkuu wa Octoba mwaka huu.

Rais Samia amesema, hadi sasa vitongoji 641 kati ya 712 vya wilaya hiyo vimeunganishwa umeme hivyo vinavyobaki vitaendelea kuunganishwa hadi vyote vikamilike.

'kwa sasa vijiji vyote nchini vimeunganishwa umeme na mbarali ikiwemo. Kwa sasa kazi iliyobaki ni kuunganisha vitongoji vyote nchini'. Rais Samia amesema.





SERIKALI KUNUNUA SHAMBA LA 'MBARALI ESTATES' KUWAGAWIA WANANCHI

Mgombea Urais kupitia Chama Cha Mapinduzi(CCM) na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dkt Samia Hassan Suluhu amesema iwapo atachaguliwa kwa kipindi kingine serikali yake itanunua shamba la 'Mbalali estate' na kuwagawia wananchi ili kupunguza ufinyu wa ardhi katika wilaya hiyo.

Rais Samia ameyasema hayo leo katika wilaya alipokuwa anahutubia maelfu ya wafuasi wa CCM waliofika kusikiliza sera zake kuelekea uchaguzi wa mwaka huu utakaofanyika Octoba 29.

Rais Samia amesema mwenye shamba amekubali kulirudisha serikalini na kwa bei nafuu na nzuri.

Katika hatua nyingine Rais Samia amesema, ili kukidhi mahitaji ya wafugaji, serikali itagawa vitalu vya ranchi ya Taifa ya NARCO ya Usangu kwa wafugaji.

Rais Samia amesema, uwepo wa wafugaji katika mkutano wake na Mabango mazuri ni kwa sababu ya kufaidika na vitalu vya ranchi hiyo.





RAIS SAMIA KUHAMISHA VIJJI VITANO MBARALI KULINDA HIFADHI YA MTO RUAHA

Mgombea Urais kupitia Chama Cha Mapinduzi (CCM) na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dkt Samia Suluhu Hassan amesema atakapopewa ridhaa ya kuongoza kipindi kingine atahamisha vijji vitano katika wilaya ya Mbarali ili kulinda hifadhi ya mto Ruaha.

Rais Samia ameyasema hayo leo wakati akihutubia maelfu ya wafuasi wa CCM wilayani Mbarali katika mkutano wake wa mwisho jijini Mbeya.

Rais Samia amesema, kuhamisha vijji hivyo vitano kunatokana na ukweli kuwa hifadhi ya mto Ruaha ndo chanzo cha maji ya mabwawa ya Mtera, Kidatu na Mwalimu Nyerere.

Ameongeza kusema kuwa iwapo serikali itaacha wananchi kufanya shughuli zao katika hifadhi hizo juhudi inazozifanya serikali kuwekeza katika miundo mbinu ya maji na umeme itakuwa kazi bure.

Rais Samia amesema serikali itafanya tathmini ya kina kuwalipa wote watakaohamishwa ili haki yao iweze kupatikana.





WANANCHI WA MBARALI WAONESHA IMANI KUBWA KWA RAIS DKT. SAMIA



Mgombea Urais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kupitia Chama Cha Mapinduzi (CCM), Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan alipowasili na kupokelewa na maelfu ya waanchi wa Mbarali katika Uwanja wa Ubungo uliopo Ubaruku, Mbarali mkoani Mbeya, kwa ajili ya kuhutubia wananchi katika kampeni za CCM.

Maelfu ya wananchi wameendelea kuonesha ukubwa wa CCM na kukubalika kwa Mgombea wao Dkt. Samia kwa wao kujitokeza kwa wingi katika kila mahali alipotia hatua zake.

Rais Dkt. Samia yupo mkoani Mbeya kwa ajili ya mikutano ya kampeni ya kunadi sera za CCM kuelekea uchaguzi mkuu utakaofanyika mwezi Oktoba tarehe 29 mwaka huu.

VIBE LA WASANII NA BALOZI MIGIRO







RAIS SAMIA KUFUFUA ZAO LA CHAI NJOMBE

Mgombea urais kupitia Chama Cha Mapinduzi (CCM) na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania amsesema iwapo atachaguliwa tena kipindi kingine serikali yake itafufua zao la chai mkoani Njombe.

Akihutubia maelfu ya wananchi walifurika kumsikiliza leo mjini Njombe Rais Samia amesema serikali imeanza kumwezesha mwekezaji kutoka Kenya kwa kumwekea mazingira mazuri ili apate fedha za kulipa madeni na kufufua kiwanda cha chai.

Rais Samia amesema mwekezaji huyu anawekewa mazingiea mazuri kwa sababu aliteteleka kidogo hivyo serikali inao wajibu wa kuhakikisha anaendelea na uzalishaji.

Sambamba na hilo, Rais Samia amesema mwekezaji huo mazingira yake yakitengamaa atalipa na malimbikizo ya mishahara ya wafanyakazi na hela zao za mifuko ya jamii ambazo hazijalipwa.

Katika hatua nyingine Rais Samia amesema serikali itahakikisha viwanda vya Lupondo na Ikanga vinafungwa vifaa vya kisasa na kufufuliwa ili kuongeza uzalishaji wa zao la chai mkoani humo.





NCHIMBI: MAENEO MAALUM KUTENGWA KWA AJILI YA WACHIMBAJI WADOGO

Mgombea mwenza kwa tiketi ya CCM Balozi Emmanuel Nchimbi amesema Dkt. Samia Suluhu Hassan anaelewa mchango mkubwa wa wachimbaji wadogo kwenye uchumi wa nchi. Ndiyo maana kupitia Ilani ya CCM 2025-2030, maeneo maalumu yatatengwa kwa ajili yao.

Kutoka kwa wachimbaji wadogo tunapata wachimbaji wakubwa, tunapata kodi ya taifa, tunapata miradi ya maendeleo.

Oktoba 29 tunasema Ndiyo kwa Samia, ili kila mchimbaji mdogo awe na nafasi ya kukua na kufanikisha ndoto zake pamoja na ndoto za Tanzania.





KILIO CHA HOSPITALI YA WILAYA YA MBOGWE, KIMESIKIKA

Mgombea mwenza kwa tiketi ya CCM Balozi Emmanuel Nchimbi Kwa muda mrefu, Hospitali ya Wilaya haijawa na uwezo wa kutosha kuhudumia wananchi wote. Changamoto za miundombinu, vifaa tiba na uhaba wa wataalamu zimekuwa mzigo mkubwa kwa familia nyingi.

Dkt. Samia Suluhu Hassan ameahidi kubadilisha hali hii. Serikali ya CCM 2025-2030 itaiboresha, kuikarabati na kuipanua Hospitali ya Wilaya ya Mbogwe ili iwe na majengo bora, vifaa tiba vya kisasa na wahudumu wa kutosha kuhudumia kila mwananchi.

Huu ndio muda wa kuhakikisha kila Mtanzania anapata huduma bora za afya bila vikwazo. Oktoba 29 tunatiki kwa Dkt. Samia - kwa afya ya watu wote!





RAIS SAMIA: MRADI MPYA WA LIGANGA NA MCHUCHUMA KUANZA KAZI BAADA YA UCHAGUZI



Mgombea urais kupitia Chama Cha Mapinduzi (CCM) na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dkt Samia Suluhu Hassan amesema iwapo atapewa ridhaa ya kuongoza tena atahakikisha mradi wa Liganga na Mchuchuma unaanza kazi baada ya uchaguzi.

Rais Samia ameyasema hayo leo wakati akihutubia maelfu ya wananchi waliofurika kumsikiliza mjini Njombe.

Amesema mwekezaji ameishapatikana na kuna mchakato unaendelea kuhakikisha mradi unafanya vizuri na kutoa ajira kwa vijana wa Kitanzania



REKODI YA UTEKELEZAJI WA MIRADI YA MAENDELEO KUMBEBE RAIS SAMIA RUNGWE

Waziri wa Habari Utamaduni, Sanaa na Michezo, Prof. Palamagamba Kabudi, amesema kuwa rekodi ya mageuzi makubwa ya maendeleo na uchumi aliyoiweka Rais Samia, ndani ya miaka minne na miezi sita akiwa madarakani ndio inafanya kusimama kifua mbele kumnadi kwa nafasi ya Urais.

Prof. Kabudi, amesema hayo kwenye mkutano wa kampeni za Uchaguzi Mkuu uliofanyika Rungwe mkoani Mbeya Septemba 5, 2025.

Miongoni mwa mambo makubwa aliyofanya kwenye jimbo la Rungwe ni pamoja na mapinduzi makubwa kwenye sekta ya kilimo hususani katika mazao ya ndizi, maharage, kahawa, chai, parachichi, na kakao ambapo Serikali ya Awamu ya Sita imewezesha wakulima kupata mbegu bora.

“Jambo jingine ambalo Mhe. Dkt. Samia amelifanya ni kuwapatia wakulima ruzuku, pembejeo bora kitu kilichopelekea kuleta tija katika uzalishaji wa mazao na kuongezeka na pia kushughulikia masoko ya uhakika ya mazao,” Prof. Kabudi, amesema.

“Nawaonea wivu sana wanarungwe kwa kupata barabara nyingi za lami mpaka vijijini ambazo ni pamoja na; barabara ya Ndulilo – Utete ambayo ina taa, barabara ya lami na yenye taa Busekelo, Rwangwa - Kyejo, na haya yanaonesha amesimamia mapinduzi ya kilimo,” amesema Prof Kabudi.

“Katika Awamu ya Tatu ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano ilifanya kazi kubwa sana kwa kujenga vituo vya afya 46, Awamu ya Nne imejenga vituo 105, Awamu ya Tano vituo 446 na katika Awamu ya Sita vituo 1,000. Atubezi kazi za watangulizi waliopita bali tunataka kuonesha mambo makubwa yaliyofanywa kwa awamu hii ili ifikapo Oktoba 29, kura zote kwa Mhe.Samia,” Prof. Kabudi amesema.

Prof. Kabudi, ameongeza kuwa ndani ya kipindi cha uongozi wa Mhe.Samia, ameimarisha miundombinu ya usafirishaji na nchi jirani ya Malawi, nakuongeza kuwa Serikali ilifungua stendi ya mabasi Tukuyu, na miundombinu ya bandari Itundi ambayo uwepo wake umeongeza biashara.

Pia, Mhe. Samia ameanza utaratibu wa kupata umeme kupitia joto ardhi nakuongeza suala hilo liko katika hatua nzuri na kuwa wanufaika wa kwanza watakuwa wanarungwe.





KONA YA ILANI

Kuboresha maisha ya
watu na ustawi wa jamii.

MAKETE

YAONGOZA KITAIFA KWA USAMBAZAJI MAJI

Mgombea ubunge wa jimbo la Makete kwa tiketi ya Chama cha Mapinduzi (CCM), Festo Sanga, amesema kuwa tangu Mhe. Samia Suluhu Hassan ndani ya miaka minne ya uongozi wa Mhe. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, jimbo la Makete linaongoza kitaifa kwa 99.8% katika usambazaji wa huduma ya maji kwa wananchi.

Amesema hayo katika mkutano wa kampeni za mgombea Urais kwa tiketi ya CCM, Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, uliofanyika Njombe tarehe 5.9.2025.

“Katika sekta ya maji kitaifa, Mhe. Sanga, amesema kwa mujibu wa ripoti ya RUWASA ya mwaka 2024, jimbo la Makete linaongoza kwa 99.8% katika usambazaji wa huduma ya maji kwa wananchi, nakuongeza kuwa hii ndio maana ya kumtua mama ndoo kichwani,” Mhe. Sanga, amesema.

Mhe. Sanga, amemshukuru Mhe. Rais kwa kazi kubwa aliyoifanya ndani ya miaka minne tangu aingie madarakani kitu ambacho kimejenga imani kwa wananchi wa Makete kwa kuendelea kumuamini.



Aidha, Mhe. Sanga, amesema toka jimbo la Makete lizaliwe kumekuwa na vituo vitatu lakini ndani ya miaka minne ya uongozi wa Mhe. Samia wamepata vituo vipya nane vya afya na kuweka historia.

Katika eneo la elimu, Mhe. Sanga, amesema kulikuwa na shule tatu lakini ndani ya kipindi cha uongozi wa Mhe. Samia shule zimeongezeka hadi kufikia 11 kwenye jimbo la Makete.

“Mhe. Rais 10.8. 2022 ulikuja kuzindua barabara ya Njombe - Makete ambapo wananchi walikuwa wakitumia siku nne. Leo hii baada ya barabara hiyo kukamilika kwa lami, wananchi wanatumia saa moja kufika safari waliyokuwa wakitumia siku nne,” amesema.

Katika jimbo ambalo bajeti ya TARURA ilikuwa shilingi bilioni 1.3 katika miaka minne umeiongeza kufikia bilioni 4 kitu ambacho kimekuwa historia kwa wilaya yetu.



**GEN S
TUNASEMA
CHAGUA
BI MKUBWA
ILI FURSA
ZIENDELEE**





KEVIN FALLEN



ssh_anatekeleza